TANGAZO LA SERIKALI NA. 655 la tarehe 18/11/2022

SHERIA YA UMEME,
(SURA YA 131)

# AMRI

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 23 and 24)*

AMRI KWA AJILI YA KUREKEBISHA BEI ZA HUDUMA YA UMEME KWA KAMPUNI YA HUSK POWER SYSTEM LIMITED YA MWAKA 2022

Jina

1. Amri hii itaitwa Amri kwa ajili ya kurekebisha Bei za Huduma ya Umeme kwa Kampuni ya Husk Power System Limited ya mwaka 2022.

Marekebisho ya bei

2. Bei za Umeme kwa ajili ya Kampuni ya Watu na Umeme Tanzania zilizoainishwa katika Jedwali la Amri hii zimeidhinishwa.

Masharti

3. Bei zilizoidhinishwa zitaambatana na masharti yafuatayo:

(a) ifikapo au kabla ya tarehe 31 Machi 2023, Husk Power System Limited iwasilishe katika Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na maji Mpango wa biashara uliopitiwa upya kwa kuzingatia bei zilizoidhinishwa; Mpango huo ujumuishe mpango wa upanuzi kuweza kuhudumia mahitaji ya wateja wa sasa na wateja wanaotarajiwa kuunganishwa baadae;

(b) ifikapo au kabla ya tarehe 31 Juni 2023, Husk Power System Limited iwasilishe kwa Mamlaka Mkataba wa Huduma kwa Wateja ili kuidhinishwa;

(c) Husk Power System Limited ihakikishe huduma inapatikana kwa masaa 24;

(d) ifikapo au kabla ya tarehe 31 Machi 2023, “Husk Power System” wawe wamebadili mfumo wa manunuzi ya umeme kuwezesha ununuzi kwa uniti kwa shilingi. Aidha, wateja

waweze kuona matumizi ya uniti zilizotumika.

(e) ifikapo au kabla ya tarehe 31 Machi, 2023, Husk Power System Limited ihakikishe mita mbovu zote za wateja zimekarabatiwa au zimebadilishwa na pia mita zinapatikana kwa matumizi ya baadae; na

(f) kila robo mwaka, Husk itaendelea kuwasilisha katika Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na maji taarifa zake za fedha na utendaji kwa mujibu wa matakwa ya Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na maji.

**JEDWALI**

*(Limetengenezwa chini ya aya 2)*

BEI ZILIZO IDHINISHWA

| Kundi la Wateja | Wakati | Bei Iliyopendekezwa (TZS/kWh) | Bei Iliyoidhinishwa (TZS/kWh) | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | 2022 | 2023 | 2024 |
| Majumbani | Mchana | 2,444 | 1,300 | 1,300 | 1,300 |
| | Usiku | 2,444 | 1,300 | 1,300 | 1,300 |
| Biashara | Mchana | 2,444 | 1,300 | 1,300 | 1,300 |
| | Usiku | 2,444 | 1,300 | 1,300 | 1,300 |

Dodoma, ……………….. 2022

MODESTUS M. LUMATO
*Mkurugenzi Mkuu*